

R_IWAWA

MWISHO WA DUNIA

**MWISHO
WA
DUNIA**

DICKSON MTALAZE

MLANGO WA KWANZA

I

Baada ya kumaliza mitihani yake ya mwisho ya chuo kikuu, Chibago Fukunyi, hakutaka kurudi kijijini kwao, Chidonghomaye, mkoani Dodoma. Aling'ang'ana jijini Dar es Salaam kwa sababu aliyachukia maisha ya kijijini. Katika miaka yake mitatu ya masomo aliyoishi jijini Dar es Salaam, Chibago alilijua jiji nje-ndani, na alikuwa ametopea kiasi cha kuonekana kama mzawa. Alivija vilabu vya pombe na kumbi za cinema, migahawa mizuri na maeneo kadha wa kadha ya kustarehe. Chibago aliyazoea maisha hayo, hivyo ikawa vigumu kwake kurudi kuishi maisha ya kutumia vibatari na kutembea umbali mrefu kuteka maji...

Aidha, Chibago alikichukia kilimo cha jembe la mkono. Tangu alipofika masomoni, alikipa mgongo, na alijua fika endapo angerudi kijijini, asingeweza kukikwepa. Akahofia kingeifubaza rangi yake ya maji ya kunde na kumpunguza kimo chake kirefu kwa kibiongo. Kukichukia kilimo ilikuwa chachu ya kumfanya asome kwa bidii, ndiyo maana licha ya kupenda starehe, hakulitupa daftari. Nje ya kuyachukia maisha ya kijijini, pia alikuwa amehakikishiwa ajira katika shule binafsi mara amalizapo masomo yake ya ualimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alipokuwa akisomea ualimu wa masomo ya fizikia na hisabati. Hivyo, kwa vyovyyote vile, hakuwa tayari kurudi kijijini kufuata kilimo na kuacha ajira mjini.

Chibago alipokuwa mwaka wa pili chuoni, alienda kufanya mazoezi kwa vitendo shule ya sekondari Jamhuri, jijini Dar es Salaam, alipokutana na mwalimu Chedego Mwaluko. Mwalimu huyo alikuwa bingwa wa somo la fizikia. Sifa zake zilivuma kila kona ya jiji la Dar es Salaam.

Mwalimu Chedego aliajiriwa katika shule hiyo ya serikali, lakini shule nyingi binafsi zilikuwa zikimwajiri kwa muda kwa ajili ya kufundisha na kuandaa *practicals*.

Usuhuba wa Chibago na Chedego uliota mizizi kwa kuwa walitoka katika kabilia moja. Hivyo Chedego akamwahidi Chibago kuwa atakapohitimu angemtafutia ajira katika shule mojawapo kati ya zile afundishazo kwani aliaminika. Kuwa na uhakika wa ajira, kulimfanya Chibago azidishe majigambo wakati alipokuwa chuoni. Wakati wenzake wakihangaika kujiuliza wangefanya nini baada ya kumaliza masomo huku wakisubiri ajira rasmi za serikali, ye ye alikuwa na uhakika wa kazi kwa asilimia zote. Aliwaringishia na kuwacheka kimoyomoyo wenzake waliokuwa wamekosa cha kufanya mjini na kubakiwa na uamuzi mmoja tu wa kurudi kijijini.

Chibago alipohitimu masomo, alipanga chumba mtaa wa Chang'ombe uliopo Tabata, jijini Dar es Salaam. Shule aliyokuwa ameahidiwa ajira ipo Tabata Kimanga, umbali mfupi kutoka Tabata Chang'ombe. Alipanga chumba cha gharama ambayo aliimudu kwa wakati huo ambao bado hakuwa na mshahara. Alitumia fedha zake za kujikimu alizokuwa akiweka akiba tangu alipokuwa chuoni. Chumba kile hakikumpendeza, lakini ilimbidi

kuishi hapo kwa muda kabla ya kutafuta makazi rasmi ambayo ndiyo aliamini yangekuwa ya hadhi yake.

Kulikuwa na wapangaji wengine wenye familia zao katika nyumba aliyopanga. Awali ilikuwa vigumu kwake kupata chumba kwenye nyumba hiyo, kwani mama mwenye nyumba hakuwa tayari kumpangisha kapera. Hata hivyo, Chibago alijitahidi kumshawishi kwa kisingizio cha kazi yake ya ualimu. Mama mwenye nyumba alikubali na kumpa masharti kedekede ambayo Chibago aliafikiana nayo. Kwanza, hakuruhusiwa kuingiza wanawake tofautitofauti chumbani mwake, pia alipaswa kufagia uwanja na kudeki choo cha nje ambacho kilikuwa kikitumiwa na wapangaji wote.

Baada ya kupata hati ya matokeo ya chuo, Chibago, alikwenda kuripoti kwenye shule aliyokuwa ameahidiwa ajira. Akatakiwa kukamilisha na kufuata taratibu zote za kiofisi kwani asingeweza kuajiriwa kinyemela. Kwanza, alitakiwa kuandika barua rasmi ya maombi ya kazi kisha kufanyiwa usaili. Chibago alifanya hivyo na kusubiri kuitwa kwenye usaili.

Siku ya usaili ilipofika, Chibago aliboronga, kwani alijiamini kupita kiasi hivyo akashindwa kuyajibu maswali muhimu kwa weledi. Jopo la usaili likamkataa licha ya kuwa na matokeo mazuri kitaaluma. Chibago hakuamini alipoyasikia majibu ya usaili. Aliamini alikuwa na kila kigezo cha kuajiriwa, hivyo alimpigia simu mwalimu Chedego na kumlaumu kuwa

hakutendewa haki lakini hakukuwa na namna nyingine ya kumsaidia. Chibago alikosa ajira!